TANGAZO LA SERIKALI NA. 24 la tarehe 17/02/2017

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

***(****Zimetungwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE ZA MWAKA 2017

Jinan a tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Mlele za mwaka 2017 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo;

Ada"au"Ushuru"maana yake ni malipo yanayotozwa na Halmashauri kwa ajili ya huduma ya uzoaji taka;

"Afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Askari" maana yake ni askari wa Jeshi la Polisi au Mgambo yeyote atakayeteuliwa au kuagizwa na Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa kutekeleza Sheria Ndogo hizi.

"Chukizo" au "Kero" maana yake ni kitu chochote

ambacho kimejengwa au kuwekwa katika hali ya uchafu na kinaweza kusababisha madhara kwa maisha ya Binadamu, adha, mazalia ya wadudu na wanyama hatari au madhara kwenye chakula na vyanzo vya maji;

“Dampo” au “Jalala” maana yake ni eneo maalum lililotangazwa kuwa limetengwa na kuhifadhiwa na Halmashauri kama eneo maalum nje ya makazi ya watu kwa ajili ya kumwaga au kutupa taka taka za aina yoyote;

“Eneo la mbele ya nyumba” maana yake ni eneo lolote la mbele ya nyumba na eneo lililoko kati ya nyumba na barabara inayopakana na nyumba hiyo au kuungana na eneo la nyumba pamoja na eneo la hifadhi ya barabara linalopisha maji ya mvua.

“Halmashauri” maana yake ni Halmashuri ya Wilaya ya Mlele;

“Huduma’ maana yake ni pamoja na usafishaji, ukusanyaji, uondoshaji na usafirishaji wa taka;

“Kaya’ maana yake ni baba mama na watoto na ni pamoja na mtu anayeishi peke yake kwa kujitegemea, watu waishio pamoja, mpangaji katika nyumba ya makazi au biashara;

“Lundo la taka” maana yake ni pamoja na vifaa na zana chakavu, mabaki ya samani ambayo haihusishi mabaki ya vifaa vya ujenzi au wanyama waliokufa wenye uzito mkubwa zaidi ya ule unaobainishwa kwenye mzigo wa taka;

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashuri na ni pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mzigo wa taka" maana yake ni pamoja na sehemu ya mabaki ya miti, vichaka, magazeti, majalada au taka ngumu zilizofungwa pamoja;

"Mmiliki" maana yake ni mmiliki wa nyumba ya makazi au biashara, taasisi, ofisi, nyumba ya biashara na ni pamoja na mpangaji, wakala au mtu yeyote mwenye dhamana ya kuishi katika nyumba;

"Nyumba ya makazi" maana yake ni pamoja na jengo lolote linalotumiwa kwa kuishi, na inajumuisha pia ardhi ambayo imetolewa kwa ajili ya kujenga nyumba ya kuishi lakini haijaendelezwa;

"Taka hatari"maana yake ni pamoja na taka zenye sumu,kemikali, taka zinazoweza kuwaka, kumeng'enyua mwili, taka zenye mionzi, au taka hatari kama ilivyobainishwa na Taasisi ya Kuhifadhi Mazingira ya Taifa na inajumuisha mafuta ya dizeli, mafuta ya taa, mafuta ya petrol, rangi, mafuta ya kuyeyushia, betri za tochi, betri za magari, madawa ya kuulia wadudu waharibifu, taka za hospitali, mafuta mazito ya kuteleza, mafuta mazito ya kulainisha au kuchanganya na vitu vingine vya viwandani, madawa ya kuulia wadudu, madawa ya kugeuzia maumbile, mizoga na maiti;

"Taka ngumu" maana yake ni aina zote za taka zinazozalishwa majumbani, kwenye taasisi, maeneo ya biashara na viwandani lakini hazihusishi maji taka au taka za kimiminika;

"Taka za majengo ya biashara" maana yake ni taka zote zinazozalishwa kutoka katika majengo ya biashara na viwanda pamoja na taka zitokanazo na utoaji wa huduma mbalimbali lakini haihusishi taka zizalishwazo majumbani;

"Ukaguzi wa kiafya" maana yake ni ukaguzi

utakaofanywa na Halmashauri au Afisa Mwidhiniwa kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria Ndogo hizi;

"Wakala" maana yake ni Kampuni, Taasisi, Kikundi jamii (CBO) au mtu yeyote aliyeteuliwa na Halmashuri kwa ajili ya kutoa huduma ya kuzoa taka katika eneo au sehemu ya eneo la Halmashauri;

4. (1.) Halmashauri itaanzisha huduma ya usafi wa mazingira na ukaguzi wa afya katika maeneo yote ya Halmashauri.

(2) Kutakuwa na Ada itakayotozwa na Halmashauri kwa ajili ya huduma za usafi wa mazingira.

(3) Ada ya ukaguzi wa kiafya italipwa na mmiliki au Mhudumu katika majengo ya biashara, vituo vya afya na zahanati za watu binafsi, famasi au maduka ya madawa, Hoteli, Mighawa, Mama/ Baba Lishe, Watoa tiba asili, Majengo ya biashara na Vioski (Groceries) na maeneo mengine kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(4) Kila mtu atakayekaguliwa kiafya na kulipa Ada ya ukaguzi wa kiafya atapewa stakabadhi ya malipo yenye nembo ya Halmashauri mara tu baada ya ukaguzi kufanyika.

Wajibu wa mmiliki wa nyumba na mpangaji

5. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba na mpangaji wa kila nyumba ya makazi au biashara:-

(a) Kuweka na kutunza vyombo vya kuweka au kutunzia taka vyenye mfuniko na mshikio kama itakavyoelekezwa na Halmashauri.

(b) Kutunza takataka zilizohifadhiwa kwenye vyombo na kuzipeleka kwenye sehemu maalum ya kukusanyia takataka ambayo ilitengwa au kupangwa na Halmashauri kwa ajili hiyo.

(c) Kutenganisha taka atakazozalisha kama vile mabaki ya chakula, karatasi, chupa, makopo na plastiki katika vyombo tofauti.

Usafi wa mazingira

6. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba, kaya au mpangaji kusafisha, kuondoa taka na kulitunza eneo lake katika hali ya usafi na madhari ambayo Halmashauri itaridhia.

(2) Bila ya kuathiri kifungu cha 5 cha Sheria Ndogo hizi itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka, kusababisha na kuruhusu taka kutupwa katika eneo lolote la jengo lake.

(3) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa taka katika maeneo ya wazi, mitaani au barabarani.

(4) Kila mmiliki na dereva wa chombo cha kusafirishia bidhaa au mizigo atahakikisha anaweka vifaa vya kufunika bidhaa au mizigo inayosafirishwa ili kutoruhusu bidhaa au mizigo hiyo kudondoka au kumwaga uchafu na kuchafua mazingira.

(5) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki na dereva wa chombo cha kusafirisha abiria kuhakikisha kwamba anaweka vyombo vya kuhifadhia taka zitakazozalishwa ndani ya gari na kuzitupa katika sehemu maalumu iliyotengwa na Halmashuri kwa ajili ya kutupa taka.

*Tangazo la Serikali Na. 24 (linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| Taratibu za kubomoa jengo | 7. | (1)Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kubomoa au kusababisha kubomoka jengo au sehemu ya jengo bila kibali cha Halmashauri.<br><br>(2)Mtu yeyote atakayeomba na kupata kibali cha kubomoa jengo au sehemu ya jengo atalazimika kuondoa mabaki ya jengo lililobomolewa kwa gharama zake mwenyewe na kutupa mabaki hayo mahali alipoelekezwa kwa mujibu wa kibali alichoomba. |
| Taratibu za uzoaji taka | 8. | (1)Itakuwa ni jukumu lakila mmiliki na mkazi wa jengo ambalo taka hatari huzalishwa kuhifadhi na kuzitupa taka hizo katika maeneo yaliyoainishwa na Halmashauri.<br>(2)Halmasahuri itaandaa utaratibu maalum wa ukusanyaji wa taka kutoka katika maeneo mbalimbali ambako taka hizo huzalishwa na kuzikusanya kisha kuzisafirisha kwa ajili ya kuzitupa katika maeneo yaliyotengwa na Halmashauri kwa ajili hiyo. |
| Utaratibu wa kulipa Ada za usafi | 9. | Halmashauri itatoza Ada yahuduma za usafi wa mazingira, ukusanyaji na uzoaji taka kwa kuzingatia viwango vya Ada vilivyoanishwa katika jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi. |
| Utaratibu maalum wa kukusanya taka | 10. | Halmashauri itaandaa utaratibu maalum ambao utakuwa wa wazi kwa wadau wote kuhusu ukusanyaji wa taka kutoka katika maeneo mbalimbali ambako taka huzalishwa na kuzikusanya kisha kuzisafirisha na kuzitupa katika maeneo yaliyoainishwa. |
| Uteuzi wa wakala | 11. | (1) Halmashauri inaweza kumteua wakala kwa ajili ya kutoa huduma ya usafishaji na ukusanyaji taka kwa niaba yake.<br>(2)Wakala atakayeteuliwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa kuhakikisha |

kuwa:-

(a) Ameingia mkataba na Halmashauri kwa ajili ya kutoa huduma ya usafi wa mazingira.

(b) Anakusanya na kutupa taka hizo kwenye dampo kuu la Halmashauri.

Ushirikishwaji wa jamii katika kuzoa na kukusanya taka

12. Bila ya kuathiri kifungu cha 10 cha Sheria Ndogo hizi, kwa ajili ya kushirikisha jamii katika shughuli za uzoaji na ukusanyaji taka, Halmashauri inaweza kukiruhusu kikundi cha kijamii kushiriki katika kazi za kukusanya na kuzoa taka katika eneo la Kata ambao kikundi hicho kinatoka au eneo lolote la Halmashauri.

13. (1)Kwa kuzingatia idadi ya watu, kiwango cha taka kinachozalishwa na utendaji kazi wa kikundi cha kijamii katika eneo ambamo kinakusanya na kuzoa taka Halmashauri inaweza:-

(a) Kukijengea uwezo kikundi hicho kwa kuruhusu kutoza ada kwa kila kaya au jengo lililopo katika eneo ambalo kikundi hicho kimepewa mkataba wa kukusanya na kuzoa taka kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

(b) Kukipa vitendea kazi na motisha nyinginezo kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wa kikundi.

(2)Endapo kikundi cha kijamii kitaomba kushirikishwa katika shughuli za kuzoa na kukusanya taka katika eneo lolote la Kata:-

(a) Shughuli za kikundi hicho zitaratibiwa na Afisa Mwidhiniwa pamoja na Afisa Mtendaji wa Kata husika na taarifa zote

za utendaji wa kikundi zitawasilishwa na kujadiliwa katika Kamati ya Maendeleo ya Kata husika.

(b) Hakitajihusisha kutoza viwango vya Ada ambavyo havikuainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

(c) Kitawasilisha taarifa ya utekelezaji wa zoezi la ukusanyaji taka na makusanyo ya Ada kutoka kila kaya, mmiliki wa jengo au familia.

(d) Kitawasilisha makusanyayo yate ya fedha ya kila siku kwa Afisa Mtendaji wa Kata ambaye atawasilisha makusanyanyo hayo kila wiki kwa Mkurugenzi.

(e) Kitapewa kibali na Halmashauri kwa ajili ya kutoza au kukusanya ada kutoka kwa kila kaya kwa ajili ya kuchangia shughuli za usafi na uzoaji taka katika kata husika.

Wajibu wa afisa mwidhiniwa

15 Bila kuathiri kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi, Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka yafuatayo :-

(a) Kutoa hati ya ukaguzi kila baada ya ukaguzi wa jengo lolote.

(b) Anaweza kutoa notisi au taarifa ya siku kumi na nne (14) ya kumtaka mtu au mmiliki wa jengo au eneo lolote kufanya usafi, marekebisho au kufunga jengo au eneo lisitumike kwa shughuli yoyote kwa sababu za kiafya au kukiuka Sheria Ndogo hizi.

*Tangazo la Serikali Na. 24 (linaendelea)*

(c) Anaweza kuingia katika eneo au jengo lolote wakati wowote kwa ajili ya ukaguzi wa majengo au maeneo ya makazi.

(d) Kukagua wahudumu wanaofanya kazi ya kutoa huduma katika majengo ya biashara , hoteli, migahawa na nyumba za kuuza vileo, nyumba za kuuza vyakula na nyumba za kulala wageni.

(e) Kuchukua hatua za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayekiuka Sheria Ndogo hizi.

Gharama za utupaji wa taka

16 Halmashauri itatoza gharama za utupaji wa taka katika jalala (dampo) kutoka kwa mawakala, wamiiliki wa taasisi mabalimbali, viwanda na makampuni pamoja na wazalishaji wengine wa taka kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi.

Marufuku

17. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi:-

(a) Kutupa taka katika maeneo ya wazi, viwanja ambavyo havijaendelezwa, barabara, mitaro au eneo lolote ambalo siyo jala (dampo),

(b) Kufuga mifugo katika

*Tangazo la Serikali Na. 24 (linaendelea)*

maeneo ya katikati ya Mji bila kibali cha Halmashauri,

(c) Kufugia mifugo katika nyumba au sehemu ya nyumba inayotumika kwa makazi.

(d) Kutoza Ada au kiwango chochote cha ada inayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi bila idhini ya Halmashauri.

(e) Kumzuia Afisa Mwidhiniwa au Mkurugenzi asitekeleze majukumu yake.

(f) Kuacha majani, makuti au matawi aliyotumia kuhifadhia au kufunika mazao katika eneo ambalo si jalala (dampo) baada ya kushusha bidhaa au mazao.

Mamlaka ya Afisa mwidhiniwa

18. Katika kutekeleza Sheria Ndogo hizi Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuzuia uingizaji wa mazao ya chakula au bidhaa nyingine sokoni au katika eneo lolote la Mamlaka ya Halmashauri ambazo zitaingizwa zikiwa zimehifadhiwa au kufunikwa kwa kutumia majani, matawi au makuti ya miti.

*Tangazo la Serikali Na. 24 (linaendelea)*

19. Mtu yeyote katika eneo la Halmashauri mwenye kumiliki nyumba, shamba, biashara au taasisi kama vile shule, Zahanati, Viwanda, Maduka, migahawa, hoteli, majengo yoyote wanapokusanyika watu, soko, minada, magulio, makanisa, misikiti, Ofisi za serikali, Ofisi za vyama mbali mbali, nyumba za kupanga ni lazima kutunza eneo lake ikiwa ni pamoja na kufanya yafuatayo;-

a) Atalazimika kuwa na choo chenye hadhi inayokubalika kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na kitahesabika kujaa kukisalia futi. 3 kufikia usawa wa sakafu ya karo.

b) Atalazimika kunyonyewa choo kikijaa na gari la maji taka kwa gharama zake mwenyewe.

c) Atalazimika kuwa na shimo la takataka au pipa la takataka pembeni mwa nyumba yake/zake au eneo la biashara na kuhakikisha takataka hizo zinaondolewa/kuchomwa mara shimo/pipa lijaapo au kufukiwa.

d) Atalazimika kuwa na karo la kuoshea vyombo (shimo la maji taka) na pia kuvuta maji hayo yanapojaa shimoni kwa gharama zake mwenyewe.

e) Atalazimika kuwa na kichanja kwa ajili ya kuanika vyombo baada ya kuoshwa.

*Tangazo la Serikali Na. 24 (linaendelea)*

Ukaguzi wa majengo

20 Itakuwa ni wajibu wa Mfanyabiashara kabla ya kuanzisha biashara kukaguliwa na Afisa mwidhinishwa.

Upimaji wa afya

21 (1) Mtu yeyote anayehusika na kuuza vyakula katika genge, jengo lolote la chakula/vinywaji anapaswa kupimwa afya yake mara moja kila mwezi na atapaswa kuwa nadhifu na mavazi safi ya sare wakati wote akiwa kazini.

(2) Kila mhudumu aliyepimwa afya yake na kuthibitishwa atapewa hati ya uthibitisho toka kwa mganga aliyempima.

(3) Ada ya Upimaji italipwa na Mpimwaji na gharama hiyo itatolewa kituo cha huduma cha Serikali, na italipwa wakati wa upimaji kwa Mganga au Afisa afya ambaye atampa stakabadhi.

Usafi katika kaya

22. (1) Kila mkazi mwenye nyumba, mmiliki au mkabidhiwa atalazimika kuwa na choo na kupalilia majani na kufagia kila mara na kutunza mazingira safi kwa umbali wa futi. 10 toka ukuta wa jengo kama ilivyo katika vipimo vilivyowekwa na kukubalika na Halmashauri.

(2) Kila mkazi mwenye nyumba, mmiliki au mkabidhiwa atapaswa kuweka jengo lake madirisha makubwa yasiyopungua 1/8 ya ukubwa wa chumba au vipimo vilivyowekwa na kukubaliwa na Halmashauri ya Wilaya.

*Tangazo la Serikali Na. 24 (linaendelea)*

Makosa

23. Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi;

1) Kufanya biashara ya kuuza vyakula vya aina yoyote barabarani, mitaani na nje ya majengo bila kuweka ndani ya kabati safi ya kioo au kufunika kwa vyombo safi kwa mwongozo wa Afisa mwidhiniwa,

2) Kuanzisha biashara ya mgahawa au genge la chakula ambalo halikutimiza masharti kama ilivyo kwenye Sheria Ndogo hizi.

3) Kuuza nyama iliyotundikwa chini ya mti au kwenye bucha ambayo si safi na haijatekeleza masharti kama yalivyo katika Sheria Ndogo hizi.

4) Kuendeleza au kusaga na kukoboa katika jengo ambalo halijatekeleza masharti ya afya na kusajiliwa.

5) Kutumia jengo lolote kwa ajili ya kuuza vyakula bila kuwa na vyoo, maji moto ya kunawa, kabati na mazingira safi.

6) Kuuza, kusambaza, kusafirisha vitafunwa, vyakula kwa kubeba katika ndoo, sufuria na au beseni hata kama vimefunikwa.

7) Kutoa huduma ya vyakula / vinywaji kubeba/kusafirisha chakula hicho kwenye buti za magari ya aina yoyote ile.

8) Kuacha maji taka kutiririka ovyo barabarani, mitaani au katika eneo la nyumba ya jirani.

9) Kuishi nyumba isiyo na choo na bafu.

10) Kutupa taka ovyo, makaratasi, maganda ya

*Tangazo la Serikali Na. 24 (linaendelea)*

matunda ya aina yoyote, uchafu wowote, mifuko ya aina yoyote.

11) Kujisaidia haja ndogo au haja kubwa katika maeneo ya wazi au mahali pasipo na choo.

*Adhabu* 24 Mtu yeyote atakaye kwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani kifungo na faini.

JEDWALI LA KWANZA
(Limetungwa chini ya Kifungu cha 4 (3))
________
Ada ya Ukaguzi wa Afya

| Na. | Aina/ Eneo la Ukaguzi | Kiwango cha Ada (Tshs.)Kwa mwezi |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba za kulala wageni (guest houses) | 5, 000/= |
| 2. | Hoteli, mighahawa , nyumba za kuuzia vyakula vilivyopikwa | 3, 000/= |
| 3. | Bucha za kuuzia nyama | 3, 000/= |
| 4 | Kibanda na maeneo ya kuchomea nyama | 1,000/= |
| 5 | Vibanda au maeneo na ya kuchomea nyama, kukaanga chips, nyama na mayai | 1,000/= |
| 6 | Kumbi za muziki, ( disks, dansi),Baa | 5,000/= |
| 7 | Vibanda vya biashara na maeneo ya biashara nyinginezo | 3,000/= |
| 8 | Maghala ya bidhaa za vyakula Vinywaji (depots | 5, 000/= |
| 9 | Nyumba za makazi na mazingira ya Nyumba za makazi | BURE |
| 10 | Maduka ya madawa baridi ya binadamu au mifugo | 5,000/= |
| 11 | Zahanati, kliniki na vituo vya Afya vya na taasisi za watu binafsi | 3,000/= |
| 12 | Maeneo ya biashara yaliyofungwa Baada ya ukaguzi wa awali na kuomba kufanyiwa ukaguzi mpya (reinspection) | 3,000/= |
| 13 | Duka au kibanda cha biashara ya jumla | 3,000/= |
| 14 | Ukaguzi wa Viosk (groceries) | 2,000/= |
| 15 | Majengo ya Taasisi | 2,000/= |
| 16 | Vyoo vya kibiashara vunavyoendeshwa na watu binafsi. | 3,000/= |
| 17 | Karakana na gereji za magari na mitambo | 3,000/= |

*Tangazo la Serikali Na. 24 (linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 18 | Karakana za vyuma na viwanda vya mbao | 2,000/= |
| 19 | Mtoa tiba Asili | 1, 000/= |

JEDWALI LA PILI

Limetungwa chini ya Kifungu cha 9

Ada ya Huduma ya Ukusanyaji na Uzoaji wa Taka.

| **Na.** | **Aina ya Biashara/ mchangiaji** | **Kiwango cha Ada kwa siku (Tshs)** |
|---|---|---|
| 1 | Mgahawa mdogo/ kibanda cha kuuzia chai au chakula | 100/= |
| 2 | Kioski na Glosari | 1,000/= |
| 3 | Nyumba ya kulala wageni (Guest house) | 1, 000/= |
| 4 | Zahanati (Taka zisizo hatari) | 1,500/= |
| 5 | Kituo cha Afya (Taka zisizo hatari) | 1,500/= |
| 6 | Mashine ya mbao katika mtaa wa viwanda vya mbao au eneo lolote lile katika Halmashauri | 500/= |
| 7 | Fundi Seremala | 100/= |
| 8 | Fundi chuma | 100/= |
| 9 | Karakana au gereji za magari | 200/= |
| 9 | Karakana nyinginezo | 200/= |
| 10 | Kiwanda kikubwa | 3,000/= |
| 11 | Kiwanda cha kati | 2,000/= |
| 12 | Kiwanda kidogo | 1000/= |
| 13 | Duka la jumla/ Super markets au mini Super markets | 500/= |
| 14 | Duka la reja-reja | 300/= |
| 15 | Shule ya Msingi ya Bweni (kwa shule za watu nataasisi binafsi) | 500/= |
| 16 | Shule ya Sekondari ya Bweni ( watu binafsi) | 500/= |
| 17 | Kituo cha kulelea watoto/ watu wenye mahitaji muhimu/ maalum | Bure |
| 18 | Duka dogo la vyakula | 300/= |
| 19 | Duka kubwa la vyakula | 500/= |
| 20 | Baa (Bar) | 1,000/= |

*Tangazo la Serikali Na. 24 (linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 21 | Kumbi za Starehe/ disko | 1,000/= |
| 22 | Klabu za usiku/ Night Clubs | 2, 000/= |
| 23 | Duka la kuuza samaki au nyama (bucha ya samaki au nyama) | 1,000/= |
| 24 | Kibanda au kituo cha Nyama choma/ chips kinachojitegemea | 500/= |
| 25 | Duka la Dawa (Jumla | 500/= |
| 26 | Duka la dawa la reja—reja | 300/= |
| 27 | Dobi | 100/= |
| 28 | Fundi cherehani | 500/= |
| 29 | Saluni ya Wanaume au Wanawake | 200/= |
| 30 | Kibanda au mwavuli wa kuuza vocha za simu | 100/= |
| 31 | Kituo cha Kuuzia nishati ya mafuta (Filling station) | 1,000/= |
| 32 | Hoteli kubwa | 1,500/= |
| 33 | Ghala (Godown) | 2,000/= |
| 34 | Kiwanda cha mashine ya kukoboa mchele/ nafaka | 1,000/= |
| 35 | Taasisi | 2,000/= |
| 36 | Washona viatu | 100/= |
| 37 | Wauza viatu vya mitumba/ dukani | 300/= |
| 38 | Wauza nguo za mitumba | 300/= |
| 39 | Toroli la bidhaa au matunda | 100/= |
| 40 | Stoo za mkaa | 100/= |
| 41 | Stoo za mbao | 200/= |
| 42 | Mama/ Baba Lishe | 200/= |
| 43 | Duka la kuuzia vipuli vya magari | 1000/= |
| 44 | Kila Kaya | 100/= |
| 45 | Gari la kushusha mizigo (Kila linaposhusha mizigo siku hiyo) | 500/= |
| 45 | Stationaries na maduka ya kuuza vitabu | 200/= |
| 46 | Duka la Dawa la Dawa baridi za binadam, duka la dawa za mifugo au pembejeo za kilimo | 100/= |
| 47. | Hospital | 1,000/= |

Jedwali la tatu

________

(Chini ya Kifungu cha 16)

Gharama za umwagaji maji taka kwenye Jalala (dampo) la Halmashauri

| **Na.** | **Kiasi cha Taka** | **Ada kwa tani** |
|---|---|---|
| 1 | Gari lenye ujazo wa tani 1 | 3,000/= |

*Tangazo la Serikali Na. 24 (linaendelea)*

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlele imebandikwa katika Sheria hizi Ndogo kutokana na Azimio la kikao cha Halmashauri ya Wilaya ya Mlele kilichoketi tarehe 17 mwezi 07 mwaka 2015 na lakiri imebandikwa mbele ya:-

GODWIN L. BENNE,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.*

DUES J. BUNDALA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.*

NAKUBALI,

Dodoma,
09 Januari, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
*Waziri wanchi-or-Tamisemi.*